# **MHUBIRI WA KIMATAIFA**

1. Kuokoka.
2. Uponyaji.
3. Amri ya kutoa pepo.
4. Miujiza.
5. Hekima.
6. Elimu
7. Mke.
8. Biblia.
9. Mamlaka ya ufalme wa Mungu.
10. Ushirika wa roho mtakatifu.
11. Yesu na malaika.
12. Mhubiri.

## 1. KUOKOKA

Jina langu ni Lameck Lister Mhubiri wa Kimataifa niliokoka mwaka 2003 mwezi wa saba au wa nane nikiwa kidato cha tatu ktk shule ya sekondari ya Kibaha mkoa wa pwani.Jambo la kushangaza wakati naokoka naliona mfano wa mwana wa mungu akiwa na umbo kama la mwanadamu mwenye nuru mithili ya njano au njano dhahabu baadaye nilikuja kufahamu ni neno la mungu akiingia ndani ya nafsi yangu, kwa leo watumishi wa mungu huita upako.

Baadaya kuona maono hayo kwa macho mawili ya damu na nyama ghafla nilijazwa furaha,amani,upendo na haki.Nikasikia yule mwana wa mungu akicheka kwa furaha,nikajiuliza nani anacheka ndani yangu wakati usoni nimenuna sina wala jambo la kunichekesha mara kile kicheko kikafurika mpaka nje yaani ktk uso nikajikuta nafungua kinywa na kucheka huku machozi ya furaha yakitoka ktk macho kama maji.Baadaye nilifahamu ni hekima,ktk mithali kwenye biblia imeandikwa

**Mithali 81 "Je! Hekima halii? Ufahamu hatoi sauti yake"?**

hekima hulia.Hivyo   nilijazwa roho mtakatifu kama Yesu kwa ajili ya utumishi. Yule aliyeniongoza sala ya kuokoka akaniambia nimshukuru mungu kwa kusema asante ghafla nikapokea karama ya kusema kwa lugha mbali na ile hekima.

Kama Yohani mbatizaji alivyosema mimi nliwabatiza kwa maji bali yeye atawabatiza kwa kiroho mtakatifu. nilijazwa roho mtakatifu baada ya kutubu kwa jina la Yesu bila kubatizwa kwa maji kama Yesu.Ila nilipata ubatizo wa maji mengi baadaye ya kupata mafundisho ya kukuliwa wokovu na kutimiliza haki yote ila nilipotabatizwa kw maji mengi sikujnazwa maana tayari

nilishajazwa hapo mwanzo upako uliikuwa ndani yangu nilishuhudia wale waminio wengine waliokuwa hawajazwa roho mtakatifu walipopata ubatizo wa maji mengi walijazwa roho mtakatifu   wakinena kwa lugha mpya ishara ya kuokoka **Marko 16:14-18.**

Siku chache baada ya kuokoka Neno la Mungu au Mungu akasema nami na kunifunulia mpango alionao juu ya maisha baadaye ulio wa amani na mwema.Akanipa ahadi na kunipanisha habari mambo ya baadaye yatakayotokea ktk maisha yangu. Neno la mungu likasema ndani yangu huku roho mtakatifu akinihakikishia kuwa ni Mungu anayema nami

Utakuwa mhubiri wa kimataifa,utajaribiwa sana,huna utayari,nitakuponya harufu, mbaya ya jasho,Utaingia mbinguni.Kwa sasa Bwana Yesu ameniponya harufu mbaya jasho,Nimejaribiwa sana njia kutoka ni kufunga ktk biblia ni maombi ya kukesha na kunijiepusha kufanya dhambi kulingana mtume **Yakabo 1:12-15** majaribu si mazuri kwa   hulenga kukuhabiria ushirika wako na mungu.hufanya hutende dhambi kuomba kuepushwa na majaribu kila siku ni muhimu maana yatoka ktk tamaa ya mwili na kwa yule mwovu.

## 2. UPONYAJI

Ni mojawapo ya karama kutoka kwa roho mtakatifu kwa ajili ya kuponya wagonjwa au roho.Ishara mojawapo inayomtambulisha mtu ameokoka.Mungu alinipa karama hiyo kwa ajili ya huduma ya mhubiri wa kimataifa aliyonipa kwa kunitamkia neno lake.

Wakati nimeokoka nikiwa mchanga kiroho silijui neno la mungu wala Biblia.Shule iilikuwa imefungwa nilimkuta mdogo wangu wa kiume Jackson Lister ndio katoka kuzliwa mdogo anasumbuliwa

na enia au ngiri mama aliniomba nimwombee nikaweka mkono ktk kinena kilichovimba na kumuombea   tangu siku ile mpaka leo hajawahi kuumwa enia amepona. Kweli Yesu ni mponyaji.

Siku ngingine ilikuwa usiku mwili wangu ulikuwa moto sana nilikuwa natetemeka ila wazo la kumwambia mama ni mgonjwa ili anipeleke hospitali halipo nilisi malaria ijapokiwa nilikuwa sijjathibitisha kwa vipimo vya hospitali.Ghafla Neno la Mungu likasema nami kwa njia ya mawazo likisema "Hivi ulipokuwa hajaoka hali kama hiyo hkikupata unaenda wapi?. nikajibu hospitali akasama omba". Baada ya chakula cha usiku nilipiga magoti na kuomba nbele za mungu aniponye kisha nikalala kuamka asubuhi niikuwa nimepona ilikuwa mwaka 2004. Kweli Yesu ni mponyaji.

Baba yangu mzazi Lister Daudi aliugua enia au ngiri kotdani ilingiia juu ya kinena ikabaki moja alikia maumivu makali hata dawa haikufaa ndipo akaniomba nimwombee nikaweka mikono juu ya kinena na kuomba saa ile ile ngiri ikashuka   kordani ikatoka kweye kinena na kurudi mahali maumivu aliyoyasikia baba yakakoma.Kweli Yesu anaweza kupoza tatizo.

Kaka eliste alikuwa aendesha usiku akaniambia nimuombee nikaweka mkono juu ya tumbo nikamwombea yesu amponye usiku ule alilala vizuri hakuamka na kwenda kuendesha ila asubuhi akasumbuliwa kidogo na kuendesha mara moja akaenda kazini jioni alirudi nikamuliza hali ya tumbo lake akasema mziima, Kweli Yesu ni mponyaji.

Kaka John alikuwa anaumwa tumbo la kawaida akiwa amelala ktk benchi nikamwombee akakubali nilipomuwekea mkono na kumwombea mara tumbo likaacha kuuma akapona palepale. Siku

nyingine nilimkuta namaumivu ya jino ametumia dawa ila bado maumivu yapo pale pale.Nikamwomba nimuombee akakubali nikaweka mkono ktk jino na kumuombea mara akawa mzima maumivu ya jino yakakoma saa ile ile. Kweli Yesu ni mpinyaji.

Mama moja alikuwa ameacha wokovu lakini mungu alimpiga fimbo alikuwa na maumivi mwili mzima ila kila hospitali aliyokwenda kupima walimwambia hawaoni ugonjwa.Mara akakumbuk alikuwa ameokoka.Alikuja kwenye kikundi cha maombi na kunieliza shida yake nikamwambia anapaswa kutubu na kurudi kanisani kuwa ushirika tena na wenzake wa kiibada alipokubali nilimwongoza sala ya toba na kumsomea **zab 103:3** kumwambia kuwa amesamehewa dhambi zake na lile tztizo litaondoka anachotakiwa kufanya ni kwenda kuungana na wenzake kwa ibada akatii siku alipotka ibadani na kurudi nyumbani akiwa na maumivu ktk mwili wake akasumumw kusoma mara akafu gua biblia na huisoma akakukuta na mstari wa biblia uliomhudumia foho alimsisitiza kuusoma kwa makini na kurudia nguvu ya mungu ikatoka ktk ule mstari na yesu aliyeniagiza kusoma biblia alimponya maumivu ya mwili yakatoweka.Kweli Yesu ni mponyaji.

## 3. AMRI YA KUTOA PEPO

Siku moja nilikuwa nimekaa ktk kalo nikimtazama mama ambaye alikuwa amembeba mdogo wangu Jackson Lister .Mara kaka John akarudj akiwa amebeba kanda ya filamu yenye jina nsuka video ya kutisha.Akiwa anamsalimu ghafla macho ya rohoni yakafumbuka nikaona pepo akitoka ktk ule mkanda na kumwingia jackson pale mdogo wangu akaanza kulia sana kila mama akimbebeleza wapi? Baada ya kuona maono hayo nilinuka na kwenda kwa mama aliyekuwa akimbembeleza mtoto kisha

nikamtazama jackson nikamwona pepo ndani yake nikamkea kwa mamlaka ya jina la yesu na mara pepo akamtoka ndipo jackson aliponyamaza kimya akaacha kulia na ishara za kipepo hazikuonekanakana ndani yake.Kweli Yesu ana mamlaka ya kutoa pepo humpa mtumishi wake anayemtuma,kumpeleka,kumweka ktk kanisa.

Rafiki yangu Yona mmoja alinichukua na kunipeleka kwa mama mmoja aliyeitwa mama Lusu aliyekuwa akisumbuliwa na pepo tulimkemea na mara yule pepo akamwacha.Kweli jina lake lina mamlaka dhidi ya pepo humpa mamlaka huyo watumishi wake kama mitume na wahubiri wa injili hata mtu aliyeokoka amtakaye.

**4. MIUJIZA**

Ni mambo yale yaliyosiyowezekana kwa wanadamu ambayo yanawezekana kwa imani na nguvu za mungu.

Palikuwa na mwanamke mmoja aliyevamiwa na majambazi na kupigwa risasi madktari walimfanyia opereshini iliwamtoe risasi ikashindikana maana risasi zilikuwa zimezama ndani ya mifupa wakamrudisha wodini nafikiri walikuwa wamepanga wamfanyie operesheni siku nyingine ,Huyo mama alikuwa mama wa rafiki yangu John Chispin ambaye alikuwa ameokoka mwenye karama ya unabii mwonaji alileta habari hiyo ktk kikundi cha maombi , Tukamwobea kesho Jioni John akaja ktk kikundi cha maombi na kushuhudia yule mama aliyepigwa risasi ilipofika asubuhi risasi zilikutwa zimetoka ktk mifupa na kukaa juu ya godoro ni muujiza na hali yake ni nzuri Yesu amemnusuru na mauti. Kweli Yesu ni miujiza.

Siku moja nilikuwa nikisaidia mama kuchota maji nikarudi nyumbani kutoka bombani chumba chetu kilikuwa kimefungwa

nilifikiri nina funguo mfukoni kumbe alikuwa nayo mama ambaye nilimwacha bombani nilijikagua mifuko yote haikuwa na funguo kwa akilindogo nikajaribu kuvuta kufuri kwa mkono haikufunguka. nikaacha na tazama nje ghafla nikajikuta nakageuka na kutazama kutazama kufuli kisha nikakazia macho kufuli kwa muda mfupi mara nikarudia tena lile zoezi la kuivuta ile naigusa ile kufuli ili ifunguke ikafunguka palepale nilistaajabia sikutumia funguo kufungua nikafungua mlango na kuingia ndani   mara mama akarudi kutoka bombani nikamuuliza funguo unayo akijibu ndiyo Kweli Yesu ni wa miujiza.

**5. HEKIMA**

Ni hali ya kutafuta tafuta na kuchunguza chunguza isiyo ya kawaida ya kibidamu maandiko matakatifu ya biblia ili kupata mema yaliyo ndani yake,mithali,ndoto ,maono na mafumbo ya mungu. Hekima ya mungu akikupa ni kwa ajili ya kumtafuta mungu wa mbinguni baba yake Yesu muumbaji na ufalme wa mungu ili utawale ktk maisha yako. Hekima ya mungu hutumika ktk kuhubiri injili,kufundisha ufalme wa mungu   na kuonya watakatifu/waliokoka.

Siku moja nikiwa ibadani kanisa namwabudu Bwana Yesu na Mungu nikasikia Sauti ya Mungu ikisema 'Hekima" kwa msusumo.Mungu alifunulia alikuwa amenipa hekima pindi nilipooka aliponijaza roho mtakatifu au upako kikarama inatambulika kama Neno la Hekima, Kweli Yesu ni mwenye Hekima yeye ni mungu mwenye hekima.

**6. ELIMU**

**Mithali 4:3**

**"Mkamate sana elimu, usimwache aende zake; Mshike, maana yeye ni uzima wako. "**

Mfalme sulemani alipewa hekima na mungu na methali ni moja ya vitabu vyake ktk hilo mungu amemsisitizia waatu wake kuhakikisha hawawi wajinga wanatakiwa waitafute elimu na waitumie ili kuwa maisha mazuri. Maisha mazuri ktk mpango wa mungu ni uzima.Ktk dunia yetu leo wengi wenye maisha mazuri au ya unafuu kidogo ili usiwe kazi isiyo ya tabu hata ya utajiri elimu ni muhimu.Wengi wenye elimu ya mungu leo na wanayoitumia ndio wanaofanya vizuri ktk wokovu/utumishi wa mungu.

Baada ya kuokoka mwaka 2003 siku chache baadaye Neno La Mungu likasema nami Utapata **divion 1:9** nikiwa kidato cha tatu kweli kidato nilipata divisione one kweli.Hapo ndipo nilipofahamu mungu anajali elimu.Kweli Yesu anajali elimu anafahamu ili niwe maisha mazuri elimu ni muhimu.Ajalbu karibu kila nilimzaa kiroho au niliyemwongoza sala ya kuokoka au nilimwombea aoke akaokoka Yesu aliwapa elimu kuwafanya wafaulu mitihani yao ya mwisho.

## 7. MKE

Mke ni ubavu mwema apewayo mwanaume na mungu. Mwanaume huyo ni mwenye ushirika mzuri na mungu kama Adamu aliyekuwa na ushirika mzuri na Mungu.Adamu hakuomba mke ila Mungu alimpeleka mke kwa adamu.

Siku moja nikiwa nimetumwa na mama kwenda dukani njiani nikasikia sauti ya mungu wangu ikisema kwa msusumo mke Ester mwaka 2004. Nilistaajabu ile sauti ilipoingia akili mwangu nilifahamu pale mungu anamzungumzi kijane wa kike jirani yetu

aliyeokoka ambaye mama yake ni mwana maombi yaani ni muombaji ameokoka wao uzao wa mwalimu wa kanisa mwenye hekima na karama zingine.

Ukweli sifa za mke kutoka kwa mungu tunazipata ktk kitabu cha Ester,sura ya mwisho ktk kitabu cha mithali na ktk nyaraka za mtume Paulo.

- Bikira
- Umbo zuri
- Uso mwema/mwema
- Mcha Mungu
- Mtii

kwa wale waliozaliwa ktk familia za waliokoka na kukua sunday school kisha kuokoka kwa mwanamke kumkuta na sifa hizo ni kawaida na heshima mbele za Yesu na mume aliyeokoka.Kwa kuwa wamekuwa ktk mafundisho ya msingi yaliyo bora kuliko wale wanaotokea dhambini na kuokoka ni vigumu kuwa na sifa hizo zote,

Mwanamke aliyeokoka anayejiandaa kuolewa yeye hutakiwa kuomba awe mtii kwa mume wake aliyeokoka ambaye mungu atampeleka,Ukiwa chini ya huduma za kinabii epuka kuolewa na mume ambaye hajaokoka.

**8. BIBLIA**

Ni kitabu kitakatifu chenye vitabu mbalimbali vya watumishi wa mungu waliotumiwa na mungu kusema na watu aliowaumba mungu ktk vizazi tofauti tofauti ktk dunia.Inaeleza uhusiano wa

mwanadamu na muumba wake pia uumbaji wa mbingu na nchi na vitu vyote vilivyomo.Maelekezo yake huweza kumsaidia mtu kumpata mungu.Ina mafundisho ya njia uziima ya kufika jambo lolote jema analohitaji mtu ktk mpango wa mungu.

Kati mwaka 2005 - 2007 nikiwa advance sekondari nasoma comb ya PCM ktk shule ya Kibaha Secondari School Mkoa wa Pwani nikiwa ktk ktk vyumba vya bweni niliikia sauti mtu aliyeaye masikioni mwangu nilitafuta bweni zima sikumuona ghafla roho akaniongoza nitoke nje ya bweni kufuatia sauti hiyo nilipotoka roho akaniongoza niangalie juu ya anga mara nikaona lango la mbinguni limefunguliwa na Yesu akatoka na kusimama juu ya anga akasema "Biblia" kwa msusumo ile sauti moja moja ilitoka kwa Yesu hadi kwenye moyo wangu ikasema na moyo wangu na roho mtakatikatifu aliye ndani yangu akishuhudia ninayemwona juu ya anga ni Yesu maono hayo yakatoweka mtu yule niliyekuwa nikimtafuta akilia sikusikia tena kilio chake.Baadaye nilikuja kufahamu yule aliye kuwa analia sio mtu bali roho mtakatifu baada kuifahamu biblia tunasoma ktk **Rum 8:26**

**"Kadhalika Roho naye hutusaidia udhaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo, lakini Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa"**

Kile kilio ni cha roho mtakatifu aliyekuwa akiomba kwa kuugua kusikoweza kutamkika mbele ile nioneshwe yesu nakupewa agizo la kusoma biblia.Ukiwa hekima na mungu unapaswa kutumia muda mwingi kusoma na kutafakari Biblia ili kumtafuta mungu na kufahamu mpango wa mungu ktkt maisha yako.

Maono hayo yakupe ufahamu hata yesu anajua yaliyoandikwa humo yanamuhusu yeye na Baba yake hivyo ili upokee neema na

nguvu zake/ upako lazima uwe na mazoea ya kuisoma. na kuitafakari bila kusahau kuitenda ili kuipata mema ya mungu kutoka mbinguni kwa njia ya maandiko matakatifu.

Biblia ni sehemu ya maisha ya mtu aliyeokoka.Uliyokoka unapaswa kutenga walau hata saa moja kila siku kuitafakari kisha kutenga muda mwingine wa kuyatenda yale uliyotafakari.

## 9. MAMLAKA YA UFALME WA MUNGU.

Ufalme wa mungu upo juu kimamlaka kuliko tawala yoyote ktk ulimwengu wa roho.Mamlaka yake ipo kinyume cha mapepo,wakuu wa giza,wakuu wa anga na falme za giza,ipo kinyume cha roho yoyote ovu au magonjwa.

Siku moja ktk maombi  mara nje ikasikika milio y musiki ya spika kubwa kama disco nikashindwa kuomba nikaamuru ile roho ya anga inayotawala mpaka kukawepo na diso iache kutenda kazi saa ile ile muziki ikazimawakaghali kuwa kamadisco kwa wakati ule mtaa ukawa kimya maazi muziki na spika za muziki ziliwekwa nje ya nyumba ktk mtaa.Ndipo nikaomba mpa nikamaliza kukiwa na hali ya utulivu.Kweli jina la Yesu lina mamlaka.

Ktk shule nilisoma nilijikuta ktk hali utafiti baada ya kuokoka kuna matatizo yalikuwa yakipata wanafunzi vidato vya mitihani ya taifa kama form two,form four na form six waliku wa hawafanyi wote mitihahani kutokana na mlipuko wa magonjw kama macho hasa malaria.Tulipokaribia mitihani ya taifa ya kidato cha nne nilimshirikisha mpendwa mmoja tukakubaliana kufunga na kuomba ili Bwana Yesu ayaepushe hayo mabaya yasiwepo ni Kweli Bwana alijibu maombi yetu tukafanya mitihani ya taifa bila mlipuko wa ugonjwa wowote. Kweli Yesu ana mamlaka ya kuzuia magonjwa.

Nilirudi shule ile baada kufaulu kidato cha tano ajabu hali ni ile magonjwa kama malaria yaliwates vidato vya mwisho vya mitihani ya taifa.Kufika kidato cha sita karibu na mtihani nikafunga peke yangu na kufanya maombi ili usitokee ugonjwa wa mlipuko wanafunzi wote wafanye mitihani ya taifa salama na Bwana Yesu akajibu maombi pia nilisikia kukuwa na kijana alishindwa kufanya mitihani ya taifa kwa sababu matatizo ya macho zaidi ya mara moja alitakiwa akafanyiwe operation india ila mwaka wetu aliweza kufanya mitihani ya taifa ya kidato sita bila matatizo ya macho kumzuia.Kweli Yesu ana mamlaka ya kuzuia magonjwa.

Siku moja usiku nikiwa nimelala nilionesha mama mmoja yupo hospitali anahangaika kujifungua bila kufanikiwa mara nikasikia sauti ya roho mtakatifu kuna uchawi sehemu za siri baada siku chache rafiki Yona akaniambia kuna mama anahitaji maombi. Tulikwenda fukamkuta mama ana mimba miezi kumi hana uchungu tukafanya maombi na kuondoka.Naamini Yesu alimhudumia vizuri na alurudi kujifungua na kupata uchungu kama sivyo rafiki angelinitafuta siku nyingne tukamwombee.Huyu ndiye mama ayetupiwa uchai sehemu za siri ili achelewe kuzaa Bwana Yesu alimuondoa.Kweli Yesu ana mamlaka ya dhidi ya uchawi.

Siku nyingine nikiwa kanisani kuna kijana mmoja na kunieleza shida yake na kutaka maombezi.Ukweli alikuwa akisumbuliwa na mwanamke aliyekuwa akivaa baibui nyeusi na kumtokea mara kwa mara na kutoweka naye hakupenda hiyo hali pengine alimwathiri ktk ndoa au ktk uhusiano wa kimapenzi.

Basi nilimwekea ktk kichwa mkono na kumwombea mara nilipoweka mikono nguvu za roho mtakatifu zikashuka na kuijaza nafsi yake nikaamuru nguvu ile ya giza imwache.Kweli Yesu ana

mamlaka ya dhidi ya nguvu za giza.

## 10. USHIRIKA WA ROHO MTAKATIFU

Ni mawasiliano kati ya mkristu aliyeokoka na mungu,yesu na malaika kwa njia ya roho mtakatifu.Roho mtakatifu huweza kuwasiliana na mkristu aliyeokoka kwa njia ya maono,ndoto,maandiko matakatifu,kutumia neno la yesu linalosemwa na watumishi mungu na kwa sauti ya ndani ya roho yako au nafsi n.k.Pia hutuombea kwa mungu kari apendavyo mungu.

Dhambi ndiyo ilizuia kuwa na ushirika na mungu kw njia ya roho mtakatifu.Ulipookoka dhambi iliondolewa kwa damu ya yesu urejeshewa ushirika na mungu kwa huyo roho mtakatifu uliyepewa.

Mimi kama mtumishi wa mungu sehemu za ushirika wa roho mtakatifu zilizorejeshwa kwangu baada ya kuokoka na ambazo mungu hutumia kuwasliana nami ni kama:

1. Maono
2. Maombi
3. Mawazo yenye kushudiwa na roho mtakatifu
4. Sauti ya Neno la hekima/Mungu,Yesu,roho mtakatifu,malaika
5. Maandiko ktk biblia
6. Neno kutoka kwa watumishi wa mungu/Yesu

Karibu watu wote waliokoka hutumia maombi kama njia ya kuwaliana na mungu na mungu hujibu maombi.Yeyote aliyeokoka

ana haki ya kuomba na kusikilizwa mbele za mungu ni mwenye haki wa mungu.Njia ya ushirika wa roho mtakatifu ya kawaida ambayo roho mtakatifu hutumia kutuombea mahitaji yetu tuliokoka mbele za mungu kama apendavyo mungu ni maombi pindi mtu uliy3okokaupigapo goti na kuomba.Mtu uliyeokoka kufahamu mungu wako anatumia njia zipi kuwasiliana nawe mbali na maombi ambayo ni general kwa wote waliokoka ni muhimu .

**11. YESU NA MALAIKA**

Kwa uzoefu wangu kuhusu malaika ambao nimewahi kuwaona kwa neema ya mungu au niliyopewa na Bwana Yesu ni wale wa nuru.

Kabla sijaokoka nikiwa shule ya sekondari Kibaha maisha yangu yakiwa ya kumcha mungu,mtenda mema na dhambi pia.Siku moja nilikuwa nimechelewa kwenda dinning hall kula wanafunzi wamemaliza kula wanatoka dinning hall mimi ndio nakwenda kula wakati marafikizangu wakinikaribia ili tupishane mara ghafla akapita katikati mfano wa mwana wa mungu kwa speed akiwa ana umbo kama la mwanadambu mwenye nuru /mwanga mithili ya njano kutoka kichwani mpaka miguuni akiwa amefunikwa huo mwanga hata ngozi haonekani full suit ya njano.Siku za uson baadaye niliokoka nakapata kufahamu ni malaika.

Siku nyingine nikiwa ibadani siku ya jumapili ilishuka nguvu ya mungu juu yangu nusura nidondoke mara macho ya rohoni yakafumbuliwa nikaona malaika wawili wamezungukwa na utaji wa nuru ya njano kwenye uso ,mikono,mabega miguu wenye kanzu nyeupe ngozi zo kama ya yesu ya kizungu wa kiisraeli wakanikaribia na kunihudumia kwa kunitoa pingu nilizokuwa nimefungwa ktk miguu ktk ulimwengu wa roho mimi mwenyewe

nilistaajabia kuona pingu ktk miguu yangu baada ya kufumbuliwa macho ya rohoni.

Hivyo hata yule niliyemwona kabla sijaokoka kama angeondoa mwanga wake yeye ni mzungu wa mbinguni kama Yesu. Kwa hiyo neema niliyopewa na mungu nimeona malaika kazi kueleza wenye rangi ya njano au full suit ya njano ktk kitabu cha ezekieli wanawaita malaika wa shaba, yaani shaba ya njano au dhahabu ya njano. Maana hao ndio wataotenda kazi ktk huduma aliyonipa Yesu na maisha yangu.

Kati mwaka 2005 - 2007 nikiwa advance sekondari nasoma comb ya PCM ktk shule ya Kibaha Secondari School Mkoa wa Pwani nikiwa ktk ktk vyumba vya bweni niliikia sauti mtu aliyeaye masikioni mwangu nilitafuta bweni zima sikumuona ghafla roho akaniongoza nitoke nje ya bweni kufuatia sauti hiyo nilipotoka roho akaniongoza niangalie juu ya anga mara nikaona lango la mbinguni limefunguliwa na Yesu akatoka na kusimama juu ya anga akasema "Biblia" kwa msusumo ile sauti moja moja ilitoka kwa Yesu hadi kwenye moyo wangu ikasema na moyo wangu na roho mtakatikatifu aliye ndani yangu akishuhudia ninayemwona juu ya anga ni Yesu maono hayo yakatoweka mtu yule niliyekuwa nikimtafuta akilia sikusikia tena kilio chake.Baadaye nilikuja kufahamu yule aliye kuwa analia sio mtu bali roho mtakatifu baada kuifahamu biblia tunasoma ktk **Rum 8:26**

**"Kadhalika Roho naye hutusaidia udhaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo, lakini Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa"**

Kile kilio ni cha roho mtakatifu aliyekuwa akiomba kwa kuugua kusikoweza kutamkika mbele ile nioneshwe yesu nakupewa agizo

la kusoma biblia.Ukiwa hekima na mungu unapaswa kutumia muda mwingi kusoma na kutafakari Biblia ili kumtafuta mungu na kufahamu mpango wa mungu ktkt maisha yako.

**12. MHUBIRI**

Ni huduma ya kanisa ambayo yesu hutumia kwenda kutafuta kilichopotea kwa kumtumia mtumishi wake aliyempa hiyo huduma k6wahubiri wenye dhambi habari njema wapate kutubu dhambi zao kwa jina lake na kujazwa roho mtakatifu yaani kuokoka.

Mfano mzuri mwa mtumishi wa yesu wa kanisa aliyekuwa na huduma moja ya mhubiri ktk biblia ni mhubiri filipo unampata ktk kitabu cha matendo ya mitume kanisa la mwanzo alilolianzisha yesu kwa kutumia mitume wake. Kama una huduma moja ya mhubiri umpewa na yesu unapaswa kumfuata Yesu aliye mhubiri aliyehubiri habari njema kwa wenye dhambi inayosema tubuni maana ufalme wa mungu umekaribia na mhubiri filipo aliyehubiri Yesu ndiye kristo.

Matendo 8;21:8 unazipata habari za mhubiri Filipo mungu alimpa amri ya kutoa pepo,karama ya uponyaji na miujiza.Mungu alimpa hekima pia kumbuka ni miongoni mwa watu 7 wenye hekima akiwemo na stephano waliochaguliwa wasimamie ugawaji wa chakula kwa wajane.

Ukiangalia karama alizopewa mhubiri filipo ndizo nilizopewa siku nilipookoka na ni hekima,miujiza na uponyaji ila pia amri ya kutoa pepo hivyo ndiyo yesu akikupa huduma ya mhubiri ya kanisa roho mtakatifu hutoa karama ya uponyaji na miujiza mungu hutoa hekima,Yesu hukupa amri ya kutoa pepo wachafu.

Kipo kitabu ktk biblia kinaitwa mhubiri ukweli lile jina la mfalme

aliyetawala mji waJ erusalemu na Israeli si kizuri kwa wahubiri waliopewa huduma na Yesu baada ya kuokoka kumbuka agano la kale kanisa halikuwepo ili usipotee kihuduma mfuate Yesu kwa watumishi waliokoka na kupewa huduma ya mhubiri na bwana yesu aliyeanzisha kanisa kumtumia mtume Petro na na wale wengine kumi na moja.

**NB: Wahubiri wa kimataifa wote walioitwa na Yesu msiogope unapaswa kuwahubiria watu wa kimataifa kama wafabiashara wa kimataifa,waandishi wa habari wa kimataifa,wanamichezo wa kimataifa wenye dhambi wapate kuokoka.**